ATD FOURTH WORLD



# RIPOTI YA TATHMINI YA MAKTABA YA MTAA 2021

# Yaliyomo

1. **Utangulizi** ........ **1**
1.1 Malengo ya zoezi la uwezeshaji ........ 1
1.2 Malengo ya tathmini ........ 3
1.3 Kamati ........ 4
1.4 Mchakato ........ 4

2. **Matokeo ya tathmini ya maktaba ya Mtaa** ........ **6**
2.1 Maana ya maktaba ya mtaa kwa mujibu wa wakazi wa Tandale ........ 6
2.2 Faida ya Maktaba ya mtaa ........ 8

3. **Changamoto** ........ **12**
3.1 Mazingira ........ 12
3.2 Uwezeshaji ........ 15

4. **Maboresho na mapendekezo** ........ **19**
4.1 Maktaba ya mtaa madhubuti ........ 19

5. **Matarajio** ........ **25**
5.1 Elimu ........ 25
5.2 Shughuli za kisanaa ........ 27
5.3 Shughuli za kuongeza kipato ........ 28

6. **Hitimisho** ........ **31**

# 1 Utangulizi

## 1.1 Maktaba ya mtaa

Maktaba ya mtaa ni eneo la wazi ambalo watoto wanaoishi katika umasikini uliokithiri hukusanyika pamoja na wenzao. Watoto hao wanatoka katika maeneo jirani na eneo linapofanyika zoezi la uwezeshaji ambalo hufanyika chini ya mti mkubwa unaoitwa "mti wa urafiki". Licha ya hivyo zoezi hili halizingatii utofauti wa kiuchumi, dini au kikabila miongoni mwa watoto pindi wakusanyikapo kwaajili ya zoezi la uwezeshaji. Hivyo wawezeshaji hutumia mbinu ambayo huwaruhusu watoto wote kuwa huru na kushiriki mipango ya mafunzo ya maktaba ya mtaa. Uratibu wa shughuli ya maktaba ya mtaa Kwa watoto hujumuisha mipango ya ujifunzaji na ufundishaji kutoka kwenye maudhui Kama vile; nyimbo, michezo kuhusu silabi na namba, kusoma hadithi miongoni mwa watoto au wawezeshaji kuwasimulia watoto, methali, maswali na majibu, vitendawili pamoja na kujifunza shughuli za sanaa katika Nyanja za uchoraji na upakaji rangi michoro. Vilevile mradi wa maktaba ya mtaa ni jumuishi Kwa kuhusisha wazazi na walezi wa watoto hao, ambapo huwa huru kujumuika pamoja na watoto wakati wa zoezi la uwezeshaji. Hata hivyo shughuli ya uwezeshaji wa Maktaba ya mtaa hufanyika mara moja Kwa wiki ambapo huwa ni siku ya jumatano katika eneo la Tandale.

*Kundi la ushauri limeundwa na marafiki wa ATD kutoka katika maeneo mbalimbali ambapo tunafanya kazi (Tegeta,/Kunduchi,Boko,Tandale na kijiji cha chole) ili kuweza kupaza sauti za uhalisia.*

# 1.2 Malengo ya zoezi la uwezeshaji la Maktaba ya Mtaa

Shughuli ya uwezeshaji wa maktaba ya mtaa ya Tandale ina madhumuni ambayo kwayo matokeo yake hukusudiwa kuonekana kwa watoto pamoja na kwa wazazi na walezi wa watoto wanaoshiriki zoezi la maktaba ya mtaa pia na kwa wanajamii wote wanaozunguka eneo la uwezeshaji. Zoezi la uwezeshaji wa maktaba ya mtaa lina malengo yafuatayo.

Maktaba ya mtaa hukusanya pamoja watoto wanaoishi katika umasikini uliokithiri na kujenga uhusiano wenye uimara thabiti kwa pamoja na familia zao.

Maktaba ya mtaa hukuza elimu isiyo rasmi na kuendeleza talanta Kwa watoto wanaoishi katika familia zenye mazingira duni/magumu Kwa kujifunza shughuli mbalimbali za kisanaa Kwa mfano, Sanaa ya uchoraji. Pamoja na shughuli zingine za ujifunzaji zilizopo nje ya mtaala rasmi unaotumiwa shuleni.

Maktaba ya mtaa hutoa nafasi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu kuwa na furaha, kucheza na kuimba pamoja pindi wanapokusanyika pamoja na watoto wenzao wakati wa zoezi la uwezeshaji.



## 1.3 Malengo ya tathimini ya Maktaba ya Mtaa

Mradi wa Maktaba ya mtaa umekuwepo tandale Kwa muda wa miaka takribani kumi na nane (18), tangu mwaka 2003 ambapo ulianzishwa na kikundi cha wawezeshaji ambao ni wafanyakazi wa kujitolea katika shirika la ATD dunia ya nne. Ambapo baadae zoezi hilo lilianza kuwezeshwa na vijana pamoja na marafiki wa taasisi mpaka wakati wa hivi sasa. Wawezeshaji Walipata wasaa wa kukusanyika pamoja na watoto wanaotoka katika mazingira magumu, ambapo waliweza kujifunza vitu mbalimbali pamoja na watoto hao Kwa mfano; kuchora, kusimulia hadithi pamoja na kuimba, kucheza pamoja na watoto hao. Kundi la ushauri lilijadiliana na likaona vyema kuwepo na tathimini ya mradi wa maktaba ya mtaa. Kulingana na uwepo wa mradi huo kwa muda mrefu, kupitia tathmini hii itatoa taswira ya ufaafu/uimara wa mradi sambamba na hilo, tathmini hii itaonesha dosari za mradi na mapendekezo ya namna ya kupatia ufumbuzi changamoto hizo kwa kuzingatia mawazo ya walengwa na washiriki wa mradi huu kutoka katika eneo la Tandale.

**Hivyo basi tathmini ya maktaba ya mtaa ina madhumuni haya:**

Tathimini inakusudia kupata  mawazo na mapendekezo juu ya maboresho



ya mradi wa maktaba ya mtaa kutoka kwa watoto, wazazi na wakazi wa Tandale, kulingana na ujuvi wao wa mradi wa maktaba ya mtaa kwa muda mrefu. Hivyo inaweza ikarahisisha kupata mawazo jenzi kutoka kwao kwa mustakabali wa maendeleo ya zoezi la uwezeshaji la makta ya mtaa wa Tandale.

Tathimini inakusudia kuibua changamoto zinazojitokeza kwenye utekelezwaji wa zoezi la uwezeshaji ambalo hufanyika kila juma, sambamba na hivyo zoezi hili linakusudia kuibua majawabu ya changamoto hizo.

## 1.4 Kamati ya tathimini

Kikao cha kundi la ushauri kilitoa mapendekezo ya majina ya watu watakaofanya jukumu la tathimini ya maktaba ya mtaa. Wawakilishi waliobeba jukumu la kuratibu tathimini ya mradi wa maktaba ya mtaa wapo sita: wawili ni wafanyakazi wa kujitolea wa shirika la ATD dunia ya nne, watatu ni vijana na marafiki wa ATD, mmoja ni mwakilishi wa wakazi wa Tandale ambaye ni kiongozi wa nyumba kumi (mjumbe).

## 1.5 Mchakato wa tathimini ya Maktaba ya Mtaa

Tathimini ya maktaba ya mtaa ilianza tarehe 12/2/2021 baada ya wanakamati kukutana na kuangalia namna gani tathimini hiyo inaweza kufanyika, kwa kutumia mbinu ya kugawa katika makundi. Alkadhalika mbinu hii ilikusudia wahojiwa wawe huru kuzungumza na kutoa taarifa jenzi na sahihi, Makundi hayo yaliyogawanywa yalikuwa matatu ambayo yalijumuisha: watoto, vijana na wazazi.

Tathimini ya awali ilifanyika ndani ya kipindi cha mwezi mmoja na nusu kwa kuwagawa watoto katika makundi ya rika la miaka sita hadi saba (6-7). Kisha miaka nane hadi tisa (8-9) na hatimaye miaka kumi hadi kumi na tano (10-15). Jumla ya watoto wote waliohojiwa ni themanini (80).

Tathimini ya pili ilifanywa kwa vijana, ambayo ilifanyika ndani ya mwezi mmoja kwa kuwagawa katika makundi na hatimaye kupata jumla ya makundi kumi na saba (17). Lengo la kugawa makundi ni kuhakikisha kila anayehojiwa anakuwa huru. Jumla ya vijana waliohojiwa ni ishirini na nne (21).

Tathimini ya mwisho ilikuwa ya wazazi wa watoto ambao wanaohudhuria maktaba ya mtaa ambapo ilifanyika ndani ya mwezi mmoja. Jumla ya wazazi waliohojiwa ni ishirini na tano (15). Mchakato mzima wa tathmini ya maktaba ya mtaa ulitamatishwa ndani ya miezi sita ambapo mnamo mwezi wa nane ulifikia ukomo wake.

Kamati imepanga kurejea na matokeo ya tathmini ambapo kupitia tukio litakaloweza kuwakutanisha wadau wote. Pamoja na hayo kuhusisha baadhi ya shule zilizopo katika eneo la Tandale, Vile vile baadhi ya Taasisi za ndani zitaweza kualikwa.

# 2 Matokeo ya maktaba ya Mtaa

## 2.1 Maana ya maktaba ya mtaa kwa mujibu wa wakazi wa Tandale

Maktaba ya mtaa kwa wakazi wa tandale ina maana ya kwamba, ni sehemu ya kuwapa watoto maarifa tofauti tofauti hususani wanapokuwa wanasikiliza au kuhadithia hadithi mbalimbali sambamba na tanzu zingine za masimulizi ambazo zinawajenga na kuwapa maarifa zaidi. Vilevile Maktaba ni sehemu inayowafundisha watoto na kuwaelimisha kutokana na mipango ya mafunzo mbalimbali pindi wanapokusanyika. Sawia na hayo kupitia michezo mbalimbali kwa mfano, kuvuta kamba na mengine inasaidia kuwajenga watoto kiakili na kimwili. Alikadhalika maktaba ya mtaa huwafikia watoto ambao wanaishi kwenye hali ya umasikini uliokithiri na kuwakusanya watoto hao pamoja na wengine bila ya kuzingatia tofauti zao za kidini, kabila kimaeneo pia kiuchumi. Pamoja na hayo pia maktaba ya mtaa ni sehemu ya kuwaendeleza watoto kutokana na vipawa/ vipaji walivyo navyo kwa mfano, kuchora na kupaka rangi michoro.

***"Maktaba ya mtaa imenisaidia kukamilisha ndoto zangu za baadae za kuwa mchoraji ili kumudu maisha yangu na wazazi wangu."***

***(Mtoto wa maktaba ya mtaa)***

Kupitia mchango huo watoto wanaohudhuria maktaba ya mtaa wamekuwa wakifanya vyema shuleni katika masomo ya uchoraji. Vilevile watoto wametia fora katika masomo ya stadi za lugha mathalani hii husababishwa na msingi wa masimulizi

***"Kupitia maktaba ya mtaa tunajifunza upendo na kuheshimiana"***

**(Mtoto wa maktaba ya mtaa)**

ya ngano za kale ambapo msingi mkubwa wa uwelewa wa watoto wengi husababishwa na ushiriki wao katika mipango ya uwezeshaji ya maktaba ya mtaa. Hata hivyo maktaba ya ni mradi jumuishi ambapo hutoa nafasi kwa wazazi/walezi pamoja na wawezeshaji kushiriki katika uwezeshaji.

*ATD Tanzania imefanya utafiti kwa miaka mingi kuhusiana na upatikanaji wa elimu bora. Kwa kuchunguza na kuchimbua sababu kwanini baadhi ya watoto hawahudhurii shuleni. Utafiti ulifanyika kati ya mwaka 2014 na 2015 ambapo ilibainika licha ya ada ya shule kuwa changamoto kwa watoto kuhudhuria shule. Kuna sababu zingine pia. Ripoti ya utafiti huu inapatikana kwa njia ya mkondoni kupitia:*

*http://www.atd-fourthworld.org/wp-content/upload/sites/5/2016/11/Booklet-EFA-FINAL-COMPLETE-ENG-OK-2.pdf*



## 2.2 Faida Ya Maktaba Ya Mtaa

Kutambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu pamoja na familia zao. Shughuli ya uwezeshaji ya maktaba ya mtaa imesaidia jamii pamoja na shirika la ATD dunia ya nne kutambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu, alikadhalika kuelewa madhila wanayopitia sambamba na ugumu wa maisha yao katika familia zao. Sambamba na hivyo shirika la ATD dunia ya nne limeweza kutoa mchango hai katika kusaidia watoto hao baada ya kuweza kubainika kupitia mradi huu wa maktaba ya mtaa. Ambapo watoto hao wameweza kupewa misaada ya kiutu na hasa misaada ya kuwawezesha kuendelea na masomo yao .

Vilevile kupitia maktaba ya mtaa familia zinazoishi maisha duni zimeweza kubainika ambapo, ndizo wanapotokea watoto wanaokusanyika katika eneo la uwezeshaji. Familia hizo pamoja na watoto wao wamekuwa wakishirikiana bega kwa bega na ATD dunia ya nne ili kuleta tija ya mradi



kwa watoto lakini kuwafuatilia kwa ukaribu watoto pamoja na mienendo yao. Kupitia utayarishwaji wa programu mbalimbali za kisanaa miongoni mwa watoto imeweza kuwasaidia watoto hao kuwa na uwezo wa kufanya kazi za kisanaa kwa mfano, kuchora. Watoto wengi wameweza kujifunza Sanaa kupitia mradi huu, alkadhalika wengine walikuwa na maarifa ya awali juu ya sanaa hii hivyo darasa la maktaba limekuwa kama msasa kuwafua zaidi. Hata hivyo watoto pia wameweza kujifunza Sanaa ya masimulizi mathalani huwa ni hadithi pamoja na hikaya/ hekaya ambazo huchagiza maarifa miongoni mwao pamoja na kutoa mafunzo na makanyo kwa watoto lakini na jamiii nzima kwa ujumla.

### Kusababisha mtagusano/mwingiliano miongoni mwa watoto ambao husababisha waweze kujifunza kwa pamoja.

Eneo la maktaba ya mtaa ni huru kwa kila mtoto kuweza kushiriki shughuli za uwezeshaji wa mradi. Misingi ya kiutu ambayo iliasisiwa na mwanzilishi wa shirika la ATD dunia ya nne Fr. Joseph Wresinski, inafuatwa katika utekelezwaji wa shughuli hiyo. Kupitia misingi hiyo ambayo ni ya kuzingatia utu na haki kwa kila mmoja maktaba imekuwa ni eneo pekee ambalo linakutanisha watoto kutoka katika familia tofauti tofauti ambapo huwa wanacheza, wanaimba pamoja na kujifunza shughuli za sanaa mbalimbali ikiwemo uchoraji bila ya kuwepo na utabaka kulingana na hali zao za kimaisha vivohivyo ubaguzi miongoni mwao. Mazingira hayo rafiki husababisha watoto kuweza kubadilishana mawazo zaidi na humjenga mtoto kuwa na hari ya kujiamini mathalani katika ujifunzaji na kukuza udadisi miongoni mwao.

### Kukuza uwelewa wa watoto kutokana na mipango ya mafunzo mbalimbali wanayojifunza katika shughuli ya uwezeshaji.

Watoto wengi hunufaika na mipango ya mafunzo mbalimbali ya uwezeshaji mathalani inayohusisha kujifunza masuala yanayohusu mazingira yanayowazunguka lakini na ile ya kisanaa ambapo baadhi ya hiyo hufundishwa katika elimu rasmi kwa mfano tanzu za fasihi. Kupitia mafundisho hayo watoto hukuza uwelewa wao sambamba na hivyo huweza kuwafunza watoto wenzao kuhusiana na Yale waliyojifunza wakati wa darasa la maktaba ya mtaa. Uwelewa huo wa watoto husababishwa na wawezeshaji kutumia mbinu shirikishi wakati wa ujifunzaji ambapo hulazimu kusikiliza mawazo ya mtoto na watoto huwa huru kujieleza au kutoa maoni juu ya jambo Fulani.

## Ongezeko la watoto wengi wanaohudhuria masomo shuleni

Mchango mkubwa wa uwepo wa maktaba ya mtaa katika eneo la Tandale ni kuongezeka kwa watoto wanaoenda shule hii inatokana na hamasa ya wawezeshaji kwa watoto pia kwa wazazi juu ya umuhimu wa elimu. Watoto wengi wanaohudhuria maktaba wanaenda shule na wachache ambao wako nje ya masomo kupitia hamasa ya maktaba ya mtaa wameshawishika kujiunga na masomo. Sambamba na hilo baadhi ya programu pendwa za maktaba ya mtaa ambazo huvuta umakini wa watoto kwa mfano hadithi, methali na vitendawili hufundishwa mashuleni. Hivyo watoto hushawishika kuhudhuria shuleni kwasababu ya mfanano wa baadhi ya mafunzo ambapo uwawia wepesi kuweza kujibu maswali yanayoshabihiana na kategoria/ vipengele hivyo.

## Kuunganisha wawezeshaji, shirika la ATD na wazazi/ walezi pia wakazi wa mtaa wa Tandale.

Uwepo wa maktaba ya mtaa katika mtaa wa tandale umekuwa Kama daraja ambalo limeweza kuwaunganisha wazazi na wawezeshaji ikiwemo na shirika la ATD dunia ya nne. Shughuli hii ni endelevu na imekuwa ikifanyika kwa muda mrefu ambapo kila wiki aghalabu wawezeshaji hukutana na



wazazi wakati wa uratibu wa zoezi la maktaba ya mtaa lakini kuweza kujadili masuala yao binafsi pamoja na changamoto wanazopitia katika mazingira yao duni alkadhalika kufuatilia maendeleo ya mtoto nje ya maktaba na kwa ujumla wake. Wazazi hao ambao wengi wao wamekuwa wanaishi katika mazingira magumu wamekuwa wakitoa ushirikiano wa dhati Kwa wawezeshaji vivyohivyo na Kwa shirika Ili kuweza kuwakwamua kutokana na maisha duni wanayoishi.

## Maktaba ya mtaa imekuwa kielelezo cha utu, kufahamiana na kuja pamoja kuzungumzia masuala mtambuka yanayoikumba jamii kila siku.

Licha ya zoezi la uwezeshaji Kwa watoto mradi wa maktaba ya mtaa, imetoa fursa na kuwa chanzo cha ustawi wa mahusiano mema miongoni mwa wanajamii lakini pia wahusika wa uwezeshwaji wa shughuli mbalimbali za shirika la ATD. Sambamba na hilo ukaribu wa wazazi, watoto na wengine wanaohusika katika zoezi la uwezeshaji umechagiza ukuaji na ukubalikaji wa zoezi husika ambapo imekuwa ni fursa ya kuzungumzia masuala mtambuka yanayoikumba jamii ikiwamo changamoto wanazokutana nazo kila siku pamoja na utatuzi wake. Vile vile kwenye msingi wa kufahamiana kupitia maktaba ya mtaa vijana wengi wameweza kufahamiana miongoni mwao licha ya kwamba wanatoka katika maeneo tofauti tofauti. Pia kupata nafasi ya kuwafahamu watu mbalimbali ambao ni wakazi wa eneo la Tandale. Ambapo miongoni mwao ni wazazi/ walezi wa watoto wanaohudhuria darasa la maktaba ya mtaa na wengine ni wakazi wa eneo hilo.

## Maktaba ya mtaa imewezesha Uratibu wa zoezi la upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa Kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Moja wapo ya malengo ya maktaba ya mataa ni kuzitambua familia zinazoishi katika mazingira magumu lakini kuweza kujenga ukaribu nao ili kuelekea ufumbuzi wa changamoto hizo. Kutokana na dhima hiyo suala la kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu mathalani wale ambao hawakuwa na vyeti vya kuzaliwa lilipewa kipaumbele ili kuwawezesha watoto wote waweze kupata vyeti hivyo ambavyo ni muhimu kwaajili ya matumizi ya uandikishwaji shule katika ngazi ya elimu ya msingi. Hata hivyo nyaraka hii hutumika Kama kiambatanishi katika upatikanaji wa huduma zingine za kijamii za hasa panapohusishwa utambuzi wa taarifa binafsi. Hivyo basi kupitia zoezi la uwezeshaji la maktaba ya mtaa taasisi ya ATD dunia ya nne kwa kushirikiana na wazazi iliweza kuwasaidia watoto hao kupata vyeti vya kuzaliwa.

# 3 Changamoto za Maktaba ya Mtaa

Licha ya uwepo wa mafanikio yaliyosababishwa na matokeo ya mradi wa uwezeshaji wa maktaba, ambao umekuwa ukifanyika katika eneo la Tandale kwa zaidi ya miaka 18 kuna baadhi ya changamoto zinazokumba mradi wa maktaba ya mtaa. Changamoto hizo zimeweza kuainishwa Kwa ufasaha Kwa kutokana na uendeshwaji wa zoezi la uwezeshaji la maktaba ya mtaa katika eneo la Tandale.

## 3.1 Mazingira ya eneo la uwezeshaji

### Taka zilizozagaa kwenye eneo la uwezeshaji

Eneo la maktaba ya mtaa limezungukwa na makazi ya watu ambapo eneo hilo limekuwa likiathirika na shughuli za kibinaadamu za kimazingira. Mathalani suala la utupwaji taka ambapo wakazi wanaozunguka darasa la maktaba ya mtaa wamekuwa wakitupa takataka pembeni na eneo la uwezeshaji. Taka hizo zimekuwa kero Kwa watoto ambao wanakusanyika



karibu nazo wakati wa uwezeshaji wa darasa la maktaba ya mtaa lakini ni hatarishi kwa afya za watoto hao hivyo wanaweza kupata magonjwa ya mlipuko yatokanayo na athari za mrundikano wa taka zilizopo katika eneo hilo. Alkadhalika katika eneo hilo la maktaba ya mtaa kuna taka ngumu zitokanazo na vyupa pamoja na vyuma chakavu. Kusambaa Kwa taka hizo katika eneo hilo la maktaba ya mtaa kunahatarisha watoto kuweza kudhurika mathalani kujikata kutokana na kuzagaa Kwa taka hizo hatarishi.

### Maji taka yanayochuruzika kutoka kwenye bomba lililopasuka

Kwenye eneo la uwezeshaji kuna bomba linalotoka maliwatoni ambalo limepasuka hivyo kusababisha kero Kwa watoto wanaokusanyika katika eneo la maktaba kwa ajili ya kujifunza. Watoto wengi wamekuwa wakichukizwa na harufu mbaya inayotoka katika bo mba hilo na pia maji taka ambayo huwa yanavuja kutoka katika bomba hilo. Changamoto hii ni hatarishi kwani yaweza kuwa chanzo cha maradhi mbalimbali ikiwemo kipindupindu Kwa watoto hata Kwa jamii ambayo inazunguka eneo la uwezeshaji la maktaba ya mtaa.

### Eneo la maktaba haliakisi shughuli inayofanyika wakati wa zoezi la uwezeshaji linalowahusu watoto wanaoishi katika mazingira duni

Eneo la maktaba limekuwa kapa halisadiki kile kinachofanyika, eneo hilo halina utambulisho/halijipambanui waziwazi ambapo ni vigumu



kumuonesha mtu mgeni yeyote kuwa kuna shughuli ya uwezeshaji inayofanyika katika eneo hilo. Mathalani sehemu ambazo kuna kuwa na shughuli za ujifunzaji Kwa watoto kunakuwa na vitu au viashiria vinavyolandana na kiwango cha ujifunzaji cha watoto. Kupitia hivyo watoto huweza kujifunza kwamfano,uwepo wa michoro mikubwa ya wanyama au mimea, kupakwa rangi za aina tofauti tofauti kwenye kuta zinazozunguka eneo la ujifunzaji n.k. Hivyo eneo la maktaba Kwa muda mrefu limekuwa kapa Kwa kushindwa kubainisha shughuli mahususi inayofanyika katika eneo hilo.

## Kuwepo na ugumu wa kuratibu zoezi la uwezeshaji wakati wa majira ya mvua.

Zoezi la uwezeshaji hufanyika Kwa ufanisi wakati wa kiangazi ambapo huwia wepesi Kwa watoto kuweza kukusanyika pamoja na kujifunza pamoja na watoto wenzao. Katika kipindi cha masika huwa ni vigumu kwa wawezeshaji kuratibu zoezi kutokana na watoto kunyeshewa na mvua hii inatokana na eneo la maktaba kuwa wazi na kutozibwa juu na paa. Kwa kiasi kikubwa watoto huadhirika na kikwazo hiki. Timu ya wawezeshaji wa



mradi wa maktaba ya mtaa hupangilia njia mbadala ya kuweza kuwasaidia watoto ili waweze kushiriki programu za darasa la maktaba ya mtaa huku wakiwa wamesalia katika kaya zao.

## 3.2 Uwezeshaji

**Kiwango kidogo cha ubunifu katika kuratibu zoezi la maktaba ya mtaa.**

Uimara wa darasa la maktaba ya mtaa hujumuisha matumizi ya mbinu mbalimbali ambazo kwazo huwezesha watoto kujifunza Kwa wepesi na wawezeshaji kuweza kutoa maarifa yenye tija Kwa watoto wanaohudhuria darasa la maktaba ya mtaa. Uratibu wa darasa la maktaba ya mtaa umekuwa na upungufu wa ubunifu hususani Kwa wawezeshaji ambapo inawalazimu kurudia njia za uawilishaji/ufikishwaji wa maarifa kwa watoto kila mara wakati wa darasa la maktaba ya mtaa. Kikwazo hiki kinadumaza ukuaji wa mradi wa maktaba ya mtaa na kupunguza tija yake kwa watoto wanaoishi katika mazingira duni, kupata maarifa mbalimbali yatokanayo na mafunzo



ya darasa la maktaba ya mtaa. Licha ya hivyo pia kumekuwa na urudiwaji wa nakala za hadithi na vitabu vingine vya masimulizi.

Kitendo hiki kinadhihirisha bayana upungufu wa ubunifu na mbinu mpya za ufundishaji na ujifunzaji miongoni mwa wawezeshaji wa mradi. Watoto wengi wamekuwa wakilalamikia kitendo cha urudiwaji wa vitabu hivyo vya masimulizi, hivyo hupunguza ufanisi wa mradi Kwa watoto wenye uhitaji. Alkadhalika muda unaotumika katika kipengele cha usomaji wa hadithi ni finyu mno.

> *" huwa tunasoma vitabu vilevile mara kwa mara "*
> **(Mtoto)**

**Wazazi wengi hawajui dhima ya maktaba ya mtaa katika eneo wanaloishi.**

Licha ya kuwa mradi wa maktaba ya mtaa umekuwepo Kwa takribani miaka kumi na nane (18) katika eneo la Tandale lakini wazazi wengi kutoka katika



mitaa ya (pakacha na muungano) hawatambui vyema maana ya maktaba ya mtaa. Wazazi wengi kutoka katika maeneo hayo wanajua maktaba ya mtaa ni eneo la watoto kucheza na kuchora tu au kufananisha maktaba ya mtaa na shule. Kutokufamu Kwa wazazi kuhusiana na maana ya maktaba ya mtaa inawia vigumu wawezeshaji kuweza kupata ushirikiano wanaoutaka kutoka Kwa baadhi ya wazazi mathalani wakati wa uratibu wa zoezi la maktaba ya mtaa.

### Upungufu wa vifaa wezeshi kwaajili ya kufanya shughuli ya maktaba ya mtaa.

Shughuli ya uwezeshaji hufanikishwa na uwepo wa vifaa wezeshi vya kutosha kwa watoto ambapo kupitia vifaa hivyo watoto huweza kujifunza. Alkadhalika wawezeshaji huweza kuwasilisha mafunzo yao kwa watoto kupitia vifaa hivyo. Zoezi la uwezeshaji wa maktaba ya mtaa linakumbwa na upungufu wa vitendea kazi ambavyo ndio msingi mkuu wa kuwezesha mradi wa maktaba ya mtaa na kuleta tija kwa watoto wanaotoka katika mazingira magumu. Baadhi ya vifaa ambavyo vina upungufu katika mradi wa maktaba ya mtaa ni: vitabu mikeka, vifaa vya uchoraji, na vibao vya kuchorea.



Upungufu huu wa vitendea kazi vya uwezeshaji wa maktaba ya mtaa husababishwa na ongezeko la mara kwa mara la watoto kutoka katika maeneo jirani na eneo la maktaba ya mtaa. Ambapo hukusanyika na watoto wenzao na kujifunza pamoja hivyo hitaji la vifaa wezeshi kwaajili ya mradi pia huongezeka mara dufu.

### Muda mchache wa uwezeshaji wa maktaba ya mtaa.

Zoezi la maktaba ya mtaa hufanyika mara moja kwa juma zima ambapo huwa ni siku ya jumatano ya juma. Wazazi hutegemea maktaba ya mtaa inaweza kuwa chachu ya watoto wao kupenda kujifunza na kujisomea zaidi wazazi hutarajia kupitia maktaba ya mtaa watoto wanaweza kujifunza maarifa tofauti tofauti mathalani shughuli za sanaa kwa vitendo. Pia maktaba ya mtaa ni darasa huru kwa watoto ambao hawajaanza shule na wale ambao wameacha shule. Lakini muda uliotengwa kufanya darasa la maktaba ya mtaa ni hafifu ambapo hautoshelezi kuongeza ufanisi wa mradi na kuleta tija, kwa watoto kuweza kujifunza pamoja.

### Wawezeshaji kutokuwa na maarifa ya kutosha ya namna ya kuratibu zoezi la maktaba ya mtaa kwa ufanisi.

Uratibu wa maktaba ya mtaa unahitaji maarifa na kutambua namna nzuri ya kuwasilisha maarifa kwa watoto ambao ndio walengwa. Baadhi ya wawezeshaji hawana maarifa ya kutosha ambayo yanaweza kuwasaidia kuhawilisha mafunzo kwa watoto sawia na kuweza kung'amua changamoto za mmoja mmoja katika msingi wa ujifunzaji na kujua namana ya kuweza kumsaidia ili aweze kupata maarifa lengwa kulingana na maudhui husika. Hivyo basi huwia vigumu Kwa wawezeshaji kuweza kuwasaidia watoto mathalani wale wenye uwelewa wa chini ambao huitaji umakini wa hali ya juu ili kuweza kuwasaidi na kuweza kujifunza kwapamoja na wenzao.

### Kutokuwezeshwa Kwa wawezeshaji wa mradi wa maktaba ya mtaa.

Wawezeshaji hutarajia baada ya kitambo kupita katika shughuli ya uwezeshaji wa maktaba ya mtaa, kuweza kuwezeshwa kila mmoja kwa kupata maarifa kupitia mafunzo rasmi katika vyuo vya ufundi. Ambapo yatakuwa ni msingi wa kuendesha maisha yao ya baadae na kuweza kujiingizia kipato kupitia mafunzo yao katika shughuli zao. Baadhi ya Vijana ambao walikuwa wakiwezesha zoezi la maktaba ya mtaa katika kipindi cha nyuma waliamua kusitisha ushiriki wao kutokana na kutokuwepo na uwezeshwaji miongoni mwao pindi walipohitaji kufanyiwa hivyo, ili kuweza kukidhi mahitaji yao na familia zao.

# 4 Mapendekezo

Kulingana na uanishwaji wa changamoto zinazokabili zoezi la uwezeshaji la maktaba ya mtaa sambamba na mazingira ya eneo linalotumika Kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli hiyo katika mtaa wa Tandale. Hivyo maboresho/marekebisho ya uratibu wa zoezi pamoja na mazingira kwa ujumla yameweza kutolewa kama ilivyo ada ili kuongeza ufanisi wa mradi miongoni mwa watoto wanaoshiriki shughuli za uwezeshaji katika mtaa wa Tandale.

## Kuongeza vifaa vya uwezeshaji katika darasa la maktaba ya mtaa

Ufanisi wa zoezi la uwezeshaji la maktaba ya mtaa hutokana na uwepo wa vifaa vyote ambavyo huitajika wakati wa zoezi la uwezeshaji. Vilevile vifaa hivyo ndivyo ambavyo hurahisisha mchakato wa uhawilishaji/ufikishwaji wa maarifa kutoka kwa wawezeshaji kwenda kwa mtoto. Hivyo basi ili kuweza kuwa na maktaba yenye ufanisi ni muhimu kuongeza vifaa vya uwezeshaji wa mradi kama vie: mikeka, vifaa vya uchoraji (penseli, penseli za rangi, vichongeo, vifutio na karatasi kubwa za kuchorea).



Utoshelevu wa vifaa hivi utaleta tija na matokeo chanya kwa watoto ambao hushiriki katika mradi huu.

### Kuwepo na maadhimisho ya siku ya familia

Maadhimisho ya siku ya familia yatasababisha manufaa kadha wa kadha miongoni mwa wakazi wa Tandale na watendaji wa shirika la ATD dunia ya nne. Miongoni mwa matokeo chanya ambayo yanaweza kuletwa na maadhimisho haya ni kuimarika kwa ushirikiano miongoni mwa wazazi na wawezeshaji wa mradi wa maktaba ya mtaa pamoja na shirika la ATD dunia ya nne kwa ujumla. Alkadhalika kuweza kutambua familia zinazoishi katika umasikini uliokithiri lakini kuweza kutambua changamoto wanazokabiliana nazo katika mazingira yao kila siku, hivyo shirika kuweza kujua namna ya kuweza kuwakwamua kutoka katika lindi hilo.

### Kuanzisha uratibu wa safari za mafunzo kwa watoto.

Kupitia safari hizo mtoto ataweza kujifunza na kujiongezea maarifa zaidi. Safari za kimafunzo zinaweza kugawanyika katika makundi mawili, mosi



safari ambazo watoto wataweza kuongeza maarifa yanayotokana na masomo ya darasani yanayofundishwa shuleni.

Aidha watoto wataweza kujifunza kupitia safari za mafunzo kuongeza ujuzi katika mafunzo ya mtaala wa ziada kwamfano, shughuli za kisanaa mathali uchoraji, upakaji rangi n.k. Sawia na hivyo pia kuweza kupata wasaa wa kuvinjari na kufurahi pamoja kama watoto.

### Mazingira yanayozunguka maktaba ya mtaa yaboreshwe

Eneo la maktaba ya mtaa linapaswa kuboreshwa ili liweze kuwa eneo rafiki kwa watoto kuweza kujifunza kwapamoja bila ya kuweza kupata madhara ya namna yoyote yale. Marekebisho ya eneo la maktaba ya mtaa yanalenga mathali kona vifuatavyo. Kutafutwa Kwa namna rafiki ya kuhifadhi taka zinazozagaa karibu na kusanyiko la watoto wakati wa zoezi la uwezeshaji.

Vilevile kudhibiti bomba la maliwato lililopasuka ambalo limepita katika eneo ambalo watoto hukusanyika na kujifunza.



Alkadhalika kutafuta namna ya kuweka paa la muda mrefu au muda mfupi kwaajili ya kujikinga na mvua mathalani katika majira ya mvua (masika). Hata hivyo eneo la maktaba ya mtaa linapaswa kupambwa na kusadifu shughuli ya ujifunzaji Kwa watoto ambayo hufanyika katika maeneo hayo. Ambapo huweza kuwavutia watoto kukusanyika mahali hapo lakini kujihisi huru zaidi na kuweza kujifunza zaidi pamoja na watoto wenzao pindi wanapohudhuria darasa la maktaba ya mtaa.

### Kuongezwa siku za uwezeshaji wa mradi wa maktaba ya mtaa

Zoezi la maktaba ya mtaa ya Tandale limeleta matokeo chanya makubwa sana miongoni mwa watoto sawia na wazazi/walezi wa watoto hao. Watoto wengi wanaoishi katika mazingira magumu wamekuwa wanufaika wa mradi wa maktaba ya mtaa ambapo umekuwa chachu ya wao kupenda shule na kujifunza zaidi.



Mathalani siku hizo zinaweza kutumika kuweza kujifunza mambo tofauti katika maeneo mbalimbali nje na eneo la uwezeshaji.

## Kuanzishwa programu ya tapori katika eneo la maktaba ya mtaa tandale.

*Tapori ni mtando wa watoto kutoka katika maeneo, asili mbalimbali kote duniani, ambao wana kauli mbiu ya "tunataka watoto wote wapate fursa sawa". https://www.tapori.org*

Shughuli ya tapori hutoa mwongozo wa kipi cha kufanya Kwa watoto pia kuonesha juhudi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na watoto kutoka katika maeneo mbalimbali kwenye jarida. Alkadhalika tapori inawapa fursa watoto ya kuchagua wanataka wafanye nini kila siku ya uwezeshaji. Kuwepo Kwa tapori kusaidia watoto kupanuka kimawazo kupitia kujifunza kutoka Kwa watoto wenzao kutoka katika maeneo mbalimbali duniani. Alkadhalika programu hii itachagiza ukuaji wa talanta miongoni mwa watoto, mathalani katika shughuli za kisanaa sambamba na kuwajengea uwezo wa kuamua hatma Yao na jamii yao Kwa ujumla.

## Wawezehaji wapewe mafunzo ya uwezeshaji wa mradi wa maktaba ya mtaa.

Mafunzo ya namna ya kuwezesha shughuli ya maktaba ya mtaa yatawasaidia kuweza kutambua namna ya kumsaidia kila mtoto vilevile namna gani aweze kunufaika na mafunzo ya darasa la uwezeshaji. Sambamba na hayo mafunzo yatawajengea wawezeshaji maarifaa na mbinu za ujifunzaji Kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili kuongeza ufanisi na tija kwa watoto wanaohudhuria darasa la maktaba ya mtaa.

## Kuendeleza vipawa vya Sanaa miongoni mwa watoto ili kutimiza ndoto zao za baadae katika shughuli za sanaa.

Maktaba ya mtaa kupitia programu zake zinapaswa kuwa Kama kurunzi ambayo itawaongoza watoto wenye talanta ya Sanaa Kwa mfano uchoraji, maigizo ya jukwaani na upakaji rangi mathalani katika michoro.

Alkadhalika ufundishwaji wa programu hizo zinapaswa ziambatane na mafunzo ya kuwajengea watoto uwezo wa kujiamini na kuwaongezea maarifa zaidi kuhusu kazi za Sanaa. Ambapo mafunzo yatatolewa na walimu mahususi katika uga huo, wenye ubia na mradi wa uwezeshaji wa maktaba ya mtaa.



# 5 Matarajio

Kutokana na changamoto zilizoweza kubainishwa na makundi yaliyoainishwa katika andiko hili la ripoti ya tathmini ya maktaba ya mtaa pamoja na masahihisho ya nyanja mbalimbali zinazokamilisha zoezi la uwezeshaji kwa ujumla. Walengwa wa mradi wa maktaba ya mtaa wameweza kubainisha masuala mbalimbali ambayo wanatarajia shirika la ATD dunia ya nne liweze kufanya. Mathalani kulingana na changamoto za eneo lao kuna shughuli kadha wa kadha wangependa zifanyike katika eneo lao kwa mustakabali wa maendeleo yao kwa mtu mmoja mmoja na pia kwa ujumla katika jamii yao.

## 5.1 Elimu

Wakazi wa Tandale wanatarajia shirika la ATD lianzishe programu maalum za kitaaluma ambazo zitakuwa na malengo mahususi ya kiutekelezaji ili kuleta tija katika masomo ya watoto wanaoshiriki maktaba ya mtaa. Alkadhalika ni njia mojawapo ya kuhakikisha uimara wa uwepo wetu katika eneo husika.

Wakazi wa Tandale wanategemea shirika la ATD dunia ya nne lianzishe darasa la elimu ya watu wazima kwa wazazi pamoja na wakazi wa maeneo hayo.

Wazazi wa wengi Tandale wanakumbwa na changamoto ya kutokujua kusoma na kuandika. Jambo hili limeweza kudhihirika dhahiri wakati wa uratibu wa shughuli za uwezeshaji wa zoezi la maktaba ya mtaa. Alkadhalika wakati wa zoezi la ugawaji wa mitihani pamoja na mazoezi kwa watoto katika kipindi cha kuenea kwa gonjwa la UVIKO-19. Katika eneo la Tandale wazazi wengi walishindwa kuwasaidia watoto wao katika masomo yao mathalani wale watoto wa ngazi ya awali na elimu ya msingi kutokana na changamoto ya kutokujua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili fasaha. Hivyo basi wazazi wengi wanamatarajio ya kwamba shirika la ATD dunia ya nne litaweza kuratibu mafunzo na pia kuanzisha darasa la elimu ya watu wazima ili waweze kujifunza kusoma na kuandika sawia na masuala mengine.

Wazazi hao wanatarajia kupitia elimu hiyo itaweza kuwasaidia wao kuweza kuwasimamia watoto wao Kwa ukaribu hususani katika masomo ya darasani. Licha ya hayo kupitia elimu hiyo wazazi hao wataweza kupata wepesi wa kufanya shughuli mbalimbali za kujikimu na kuongeza kipato lakini kuweza kutatua changamoto za kimawasiliano baina yao na watu wengine.

Wazazi na walezi wanatoa rai ya kuanzishwa Kwa mpango wa masomo ya ziada kwaajili ya watoto wao.



Wazazi wa maeneo ya Tandale wanatarajia shirika la ATD dunia ya nne kupitia shughuli yake ya maktaba ya mtaa liweze kufungua mpango wa masomo ya ziada Kwa watoto wanaoishi katika mazingira duni ili nao waweze kupata fursa ya kujifunza zaidi mbali na maudhurio ya shuleni kila siku. Walezi/wazazi hao wameweza kuainisha ugumu ambao watoto wao wanaupitia katika kujifunza wakiwa shuleni kutokana na wingi wao katika chumba kimoja cha darasa huwawia vigumu kuweza kumwelewa mwalimu kwa wepesi hivyo huhitaji masomo ya ziada ili kuweza kujifunza zaidi.

Hata hivyo bado huwa ni changamoto kwa watoto wengi kuweza kupata nafasi ya kujifunza masomo ya ziada pamoja na wenzao mathalani wale wanaotoka katika familia duni kabisa. Hivyo basi rai na matarajio ya wazazi hao ni kuona siku moja kunaanzishwa mpango wa masomo ya ziada ambapo watoto kutoka katika familia duni nao wataweza kunufaika kitaaluma na mpango huo.

## 5.2 Shughuli za kisanaa

**Mradi wa maktaba ya mtaa uanzishe mpango wa maonesho wa shughuli zitokanazo na Sanaa ya mikono.**

Uratibu wa shughuli za maktaba ya mtaa vilevile umelenga katika kukuza na kuendeleza vipawa/vipaji vya watoto wanaotoka katika mazingira magumu. Sambamba na hivyo wazazi pamoja na watoto wanaoshiriki maktaba ya mtaa wanatarajia shirika kupitia mradi wa maktaba ya mtaa kuandaa maonesho ya kazi za Sanaa ya mikono.



Ambapo zitatoa chachu Kwa wenye talanta kufikia malengo Yao ya kisanaa na hata kwa watoto pamoja na vijana wengine kuweza kupata jukwaa la kujifunza na kuongeza maarifa kutoka kwa wasanii mbalimbali ambao wataweza kushiriki katika mpango huo.



# 5.3 Shughuli za kiuchumi

Kuanzishwa vikundi vya ujasiliamali miongoni mwa wanaume ambao ni wakazi wa eneo la Tandale.

Licha ya jitihada kubwa za kukomboa familia duni kiuchumi kupitia kutoa fursa kwa wanawake kutoka katika maeneo mbalimbali ya jiji la dar es salaam ikiwemo na Tandale, makundi mengine pia katika jamii yanauhitaji wa kufikiwa na fursa hizi za kujikwamua kutoka katika lindi la umasikini.



Alkadhalika katika ufanyikaji wa miradi hii ya ujasiliamali katika eneo la Tandale wakazi wake wanatarajia kuanzishwa kwa makundi ya wanaume ambao wataweza kupewa elimu ya ujasiriamali na kuweza kufanya kazi za uzalishaji wa bidhaa kwaajili ya mauzo kwa kulingana na mafunzo watakayokuwa wamepewa katika madarasa ya ujasiriamali.

Hata hivyo ni shauku ya wanawake wengi ambao ni wakazi wa Tandale kuona nao wakishirikishwa zaidi katika shughuli za uzalishaji ili kujikimu. Mbali ya uwepo wa kikundi cha ujasiriamali kinachonufaika na uzalishaji wa bidhaa biashara pindi ziuzwapo, bado kuna uhitaji mkubwa wa kuweza kupanua mbawa na kuweza kuwafikia wanawake wengi zaidi. Ambao wanaishi katika umasikini uliokithiri, hivyo basi matarajio ya wanawake wengi wa Tandale ni kuweza kujumuishwa katika vikundi vya ujasiriamali ili waweze kujikimu mahitaji yao na kuhudumia familia zao sambamba na kujikwamua katika lindi la umasikini.



# 6 Hitimisho

Kwa kuhitimisha tathmini ya mradi wa maktaba ya mtaa wa Tandale, ambao ulianzishwa takribani miaka 18 iliyopita umekuwa ni kurunzi adhimu ambayo imeweza kumulika mapungufu ya uratibu wa zoezi zima la maktaba ya mtaa. Sambamba na hilo mapendekezo yaliyotoka kwa walengwa wa maktaba ya mtaa pamoja na jamii inayozunguka eneo la uwezeshaji yameweza kubainishwa na kudadavuliwa kindakindaki. Alkadhalika wakazi na walezi wa watoto wanaoishi katika mazingira duni wameweza kuzungumza baadhi ya masuala mtambuka katika eneo lao ambayo sio miongoni mwa shughuli zinazofanywa na shirika.



Hivyo basi wameweza kutoa rai yao kupitia zoezi hili la tathmini na kutarajia kuwepo na utekelezwaji wa majawabu ya changamoto walizozianisha kwa wakati ujao ili kuweza kuleta tija miongoni mwao lakini pia katika jamii yao kwa ujumla. Wazazi na wakazi wameweza pia kubainisha usawa wa kijinsia katika ushiriki wa shughuli za uzalishaji mali (kiuchumi).Vilevile kutia msisitizo uwepo wa ulazima wa kuwahusisha watu wote katika jamiii kwenye shughuli za kiuchumi ili kuweza kujikwamua katika lindi la umasikini. Alkadhalika tathmini ya maktaba ya mtaa imeweza kuibua uhitaji wa vijana wawezeshaji wa mradi wa maktaba ya mtaa kuweza kuthaminiwa mchango wao wanaoutoa kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu sawia na kuweza kutambuliwa na shirika kupitia kupata fursa za masomo na uwezeshwaji wa kipato ili na wao waweze kujikwamua kutoka katika lindi la umasikini uliokithiri.



Hata hivyo baadhi ya wakazi wa Tandale wameweza kuzungumzia uhitaji wa huduma bora za kiafya mathalani upatikanaji wa bima za afya miongoni mwa familia duni ili waweze kupata uhakika wa matibabu bora pindi wapatapo maradhi. Pia kupitia tathmini hii imeweza kuonesha ulazima wa ushiri wa pamoja wa wanajamii pamoja na mashirika mengine yasiyokuwa ya kiserikali katika kutatua changamoto sugu zinazozikumba familia zinazoishi katika lindi la umasikini. Changamoto hizo zipo katika maeneo yafuatayo: elimu, afya na mazingira wanayoishi kutokana na vikwazo hivyo pia ni rai kwa shirika la ATD dunia ya nne kwapamoja na wadau wengine kupanga maeneo ya mkakati ya miradi ya kimaendeleo ili kuweza kushirikiana na familia zinazoishi katika umasikini na hatimaye kuweza kuwasaidia kujikwamua na kuleta maendeleo ya mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.



## Washiriki wa kamati ya tathmini ya programu ya maktaba ya mtaa:

Andiko la mahojiano yote linapatikana Kwa mwenye kuhitaji, andiko hili lipo kwa njia ya nakala tete na nakala ngumu. Lakini ni kwa ridhaa ya waliohojiwa na pia kuzingatia misingi ya usiri wa wahojiwa katika mchakato wa kukusanya maoni wakati wa tathmini.

- Rose Ubwe (Tandale)
- Elizabeth Peace (Tegeta)
- Godfrey Mwaja (Tandale)
- Hemedi Star (Team)
- Micol Bonapace (Team)
- Gasper Mbwambo (rafiki wa Atd)

- Kwa kushirikiana na Terry Kiarie (Kenya)

ATD
FOURTH WORLD

**AGIR TOUS
POUR LA DIGNITÉ.**

**ATD Fourth World Tanzania
Kinondoni District, Mwananyamala, Kambangwa, Igusure Street.
P.O Box 61786
www.atd-fourthworld.org**

nartive | Designed by
Nartive Kumkichwa